# SERIKALI YA KAUNTI YA KILIFI

## MPANGO UNGANISHI WA MAENDELEO YA KAUNTI: TOLEO FUPI

## LA

## 2023-2027







**MANDHARI: Uharakishaji wa Mabadiliko ya Kijamii na Uchumi kwa Ukuaji Jumuishi**

**MEI 2023**

# TAARIFA YA RUWAZA NA SHABAHA ZA KAUNTI

1






## RUWAZA

Kuwa kaunti inayoongoza, yenye uthabiti, uzalishaji wa hali ya juu, yenyeusalama na ustawi na inayotoa maisha ya hali ya juu kwa wakaazi wake wote.



## SHABAHA

Kuweka mazingira wezeshi kwa matumizi bora ya rasilimali, ukuaji wa viwanda na utoaji wa huduma muhimu kwa ufanisi kwa ajili ya kuboresha maisha kwa wote.

## MAADILI MSINGI

- Uadilifu
- Uwazi na uwajibikaji
- Matumizi ya busara ya Rasilimali za Umma
- Ujumuishwaji na Ushirikishwaji wa Umma
- Uendelevu wa Mazingira
- Kuthamini Utofauti.

# YALIYOMO, ORODHA YA MAJEDWALI, ORODHA YA TAKWIMU



# Yaliyomo

TAARIFA YA RUWAZA NA SHABAHA YA KAUNTI ....3
Orodha ya majedwali....7
Orodha ya takwimu....8
1.0 Muktadha wa CIDP III 2023-2027....9
1.1 Utangulizi....9
1.2 Muhtasari wa Jumla wa Kaunti....9
1.2.1 Hali ya kiikolojia....9
1.3 Vitengo vya utawala na siasa....11
1.3.1 Viengo vya utawala....11
1.4 Vipengee vya idadi ya watu....11
1.4.1 Idadi ya watu, muundo na maenezi....11
1.4.2 Msongamano wa watu na maenezi....12
1.4.3 Hali ya umaskini....13
2.0 Uhakiki wa utendaji wa kaunti 2018-2023....14
2.1 Uhakiki wa utendaji waCIDP II (2017-2022)....15
2.2 Uhakiki wa matumizi ya Kaunti....16
2.3Uhakiki wa utendaji wa sekta....16
2.3.1 Sekta ya afya....17
2.3.2 Sekta ya elimu....19
2.3.3 Uhifadhi wa mazingira, maji, usafi wa mazingira na maliasili....20
2.3.4 Utawala wa umma na mahusiano ya kiserikali....22
2.3.5 Sekta ya ulinzi wa jamii, utamaduni na burudani....22
2.3.6 Kilimo, maendeleo ya ufugaji na uvuvi....23
2.3.7 Ardhi, nyumba, mipango ya nje na maendeleo ya miji....23
2.3.8 Sekta ya nishati na miundo msingi....24
2.3.9 Maendeleo ya biashara, utalii, viwanda na makundi ya ushirika....24
2.4 Changamoto za utekelezaji wa CIDP II....25
2.5 Maswali ibuka katika utekelezaji wa CIDP II....25
2.6 Mafunzo kutoka kwa utekelezaji waCIDP II....25
2.7 Ukadiriaji wa maliasili za kaunti....26
2.8Masuala ya maendeleo....29
3.0 CIDP ya kaunti ya Kilifi (2023-2027)-Mawanda yatakayopewa kipaumbele....32

3.1 Mawanda yatakayopewa kipaumbele kisekta na mikakati ya 2023-2027....33
3.1.1 Huduma za afya zinazopatikana kwa urahisi na za gharama nafuu....33
3.1.2 Elimu bora....34
3.1.3 Usimamzizi wa maji, mazingira, mali asili na uthibiti wa taka yabisi....35
3.1.4 Utawala wa umma na mahusiano ya kiserikali....36
3.1.5 Ulizi wa jamii....36
3.1.6 Kilimo....38
3.1.7 Ardhi, nyumba, mipango tekelezi na maendeleo ya miji....40
3.1.8 Nishati na miundomsingi....40
3.1.9 Maendeleo ya biashara, utalii, viwanda na Vyama vya ushirika....41
3.1.1 Bunge la kaunti....41
3.2Miradi Kielelezo....42
4.0 MFUMO WA UTEKELEZAJI WA CIDP....46
4.1 Mahitaji ya kifedha ya kila sekta....47
4.1.1 Mahitaji ya kifedha ya kaunti kama asililia ya jumla ya mahitaji ya kifedha ya kaunti....47
4.2 Makadirio ya mapato....48
4.3 Mapungufu ya raslimali....49
4.3.1 Hatua za kukabiliana na upungufu wa mapato....50
5.0 Ufuatiliaji, tathmini na utoaji ripoti....52
5.1 Muundo wa ufuatiliaji na tahmini ya kaunti....52
5.2 Viashiria vya matokeo ya miradi iliyopewa kipaumbele na malengo yanayohusiana....53

# Orodha ya majedwali


Jedwali 1.1: Maeneo kwa kilomita mraba ya kaunti ndogo..........11
Jedwali 1.2: Makadirio ya idadi ya watu katika kaunti ndogo kijinsia..........12
Jedwali 1.3:Usambazaji na wingi wa watu kulingana na kaunti ndogo..........12
Jedwali 2.1:Uchanganuzi wa vyanzo vya mapato vya kaunti..........15
Jedwali 2.2:Uchanganuzi wa matumizi ya Kaunti..........16
Jedwali 2.3:Tathmini ya maliasili..........26
Jedwali 3.1: Miradi Kielelezo ya kaunti..........42
Jedwali 4.1:Mahitaji ya kifedha ya kila sekta..........47
Jedwali 4.2: Makadirio ya mapato..........48
Jedwali 5.1: Viashiria vya matokeo na malengo ya sekta ya afya..........53
Jedwali 5.2: Viashiria vya matokeo na malengo ya sekta ya elimu..........56
Jedwali 5.3: Viashiria vya matokeo na malengo katika sekta ya maji,mazingira na maliasili..........57
Jedwali 5.4: Viashiria vya matokeo na malengo katika sekta ya Utawala wa Umma na Mahusiano baina ya Serikali..........58
Jedwali 5.5: Viashiria vya matokeo na malengo katika sekta ya ukinzi wa jamii na ya bururdani..........59
Jedwali 5.6: Viashiria vya matokeo na shabaha katika sekta ya kilimo,maendeleo ya ufugaji na uvuvi..........60
Jedwali 5.7: Viashiria vya matokeo na shabahaKatika sekta ya ardhi, nyumba, mipango tekelezina maendeleo ya miji..........61
Jedwali 5.8: Viashiria vya matokeo na shabaha katika sekta ya nishati na miundomisingi..........62
Jedwali 5.9: Viashiria vya matokeo na shabaha jatika sektaya maendeleo ya biashara, utalii, viwanda na makundi ya ushirika..........63
Jedwali 5.10: Bunge la kaunti..........63
Jedwali 5.11: Mpango wa utathmini..........64

# Orodha ya Takwimu

Kielelezo 1.1:Nafasi ya Kaunti ya kilifi katika ramani ya Kenya....9
Kielelezo 1.2: Hali ya umaskini katika kaunti ya Kilifi....13
Kielelezo 2.1: Uchambuzi wa yanayotokana na kaunti dhidi ya yale yanayotoka serikali kuu....15
Kielelezo  2.2: Uchambuzi wa matumizi ya bajeti ya kaunti kisekta....16
Kielelezo 4.1: Mfumo wa utelezaji wa CIDP....46
Kielelezo  4.2: Mahitaji ya kifedha kama asilimia ya jumla ya bajeti....48
Kielelezo 4.3:Mielekeo ya makadirio na mapato....49
Kielelezo 4.4:Uchambuzi wa mapengo ya raslimali....50

# 1.0 Muktadha wa CIDP III 2023-2027

## 1.1Utangulizi

Hili ni toleo fupi la mpango jumuishi wa Maendeleo wa Kaunti ya Kilifi(2023-2027). Huu ni mpango wa maendeleo (CIDP)  wa tatu tangu kuanza kwa ugatuzi.Inafuata utekelezaji wa CIDP ya pili  (2018-2022) (2023-2027). CIDP ni zao la mashauriano mapana kati ya wadau mbalimbali katika ngazi ya Kitaifa na Kaunti.

Mpango huu wa maendeleo, unahusishwa na majukumu ya kimataifa kama vile Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ajenda ya AU 2063 na pia imeoanisha ajenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi ya “Bottom Up” kama ilivyopendekezwa katika Mpango wa nne wa Muda wa Kati (2023-2027) wa ruwaza ya Kenya 2030.

## 1.2 Muhtasari wa jumla wa kaunti

Kaunti ya Kilifi iko kati ya latitudi 2020” na 400” kusini, na kati ya longitudi 39005” na 40014” Mashariki na inachukua eneo la 12,370.8km2. Ina sifa kuu za topografia nne ambazo ni ukanda mwembamba, uwanda wa nyayo, ukanda wa pwani na Nyanda za Juu za Nyika.




*Kielelezo1.1: Nafasi ya Kaunti ya Kilifi katika ramani ya Kenya*

Kaunti hii hupata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambayo huwa na mvua ya wastani kati ya mililita 300 na mililita 1300. Viwango vya joto vya kila mwaka ni kati ya sentgrade 210 na sentigredi 300 katika ukanda wa pwani na kati ya sentigradi 300 na sentigredi 340 katika bara. Kielelezo 1.1 Knaonyesha ramani ya Kenya na eneo la Kaunti ya Kilifi.

Kielelezo1.1: Nafasi ya Kaunti ya Kilifi katika ramani ya Kenya

Kaunti ya Kilifi ina kaunti ndogo saba, tarafa 35, ofisi za usimamizi wa serikali ya kaunti 35 pamoja na wadi za uchaguzi, lokesheni 62 na lokesheni ndogo 165. Kulingana na Sensa ya KNBS ya mwaka wa 2019, Kaunti ya Kilifi ilikuwa na jumla ya wakazi 1,453,787 walio na 704, wanaume 089 na wanawake 655,673.

Kwa kawaida, idadi ya watu wenye umri mdogo iko juu kuliko watu wazee. Hivi sasa, kuna jumla ya wingi wa watu 116 kwa kila kilomita mraba ambayo inakadiriwa kuwa itaongezeka hadi watu 148 kwa kilomita mraba ifikapo 2027.Kaunti ndogo iliyo na watu wengi zaidi ni Kilifi Kusini yenye watu 713 kwa kila kilomita mraba huku Magarini na Ganze zikiwa kaunti ndogo zenye idadi chache zikiwa na watu 37 na 45 kwa kila kilomita mraba mtawalia. Katika kipindi cha miaka mitano, Kilifi Kusini na Kilifi Kaskazini zimesalia kuwa na watu wengi zaidi huku Magarini na Ganze zikisalia kuwa na idadi ndogo zaidi ya watu.

### *1.2.1 Hali za Kiikolojia*

Kaunti hii imegawanywa katika maeneomatano ya Kilimo-kiikolojia(AEZ). Maeneo haya yanarejelea maeneo yenye sifa zinazofanana na zinazohusiana na uzalishaji kama vile kupata joto la wastani kila mwaka, mimea na unyevunyevu Maeneo haya ya  yanauwezo tofauti wa kilimo. Maeneo haya ni pamoja na yafuatayo:-

**1,453,787**

Jumla ya wakazi wa Kilifi

***Maeneo ya minazi na mihogo:*** Eneo hili hupatikana katika nyanda za juu za pwani na nyanda za chini za pwani na lina uwezo wa juu zaidi wa uzalishaji wa mazao katika kaunti. Shughuli kuu za kilimo katika eneo hili ni pamoja na upandaji miti ya matunda (miembe, michungwa, mikorosho na minazi), kilimo cha mboga (pilipili, mabiringanya, mabenda) na upandaji wa mazao ya chakula (mahindi, ndizi, kunde, mpunga wa nyanda za juu, pojo). Ufugaji wa ng'ombe wa maziwa pia hufanya vizuri katika eneo hili.Eneo hili hupokea mvua ya wastani wa milimita 1,300 na halijoto ya sentigradi 240 kwa mwaka.





***Eneo la mikorosho na miembe:***Sehamu hii hunaenea kuelekea kaskazini kando ya ukanda wa pwani hadi msitu wa ArabukoSokoke. Eneo hili hupokea mvua ya wastani wa milimita900 na joto la wastani wa sentigredi 240 kila mwaka. Lina uwezo wa kilimo wa aina za mazao sawa na eneo la minazi na mihogo lakini kwa uzalishaji kidogo kidogo.

***Eneo la mtama na mifugo:***Eneo hili linauwezo mdogo wa kilimo na hupata mvua ya kila mwaka kati ya milimita 700 hadi milimita 900. Eneo hilo linafaa kwa kilimo cha ardhi kavu kinachosaidia mazao yanayostahimili ukame na mashamba ya mifugo.

***Mashamba ya Ufugaji ya nyanda za chini***:Eneo hili hutofautiana kwa urefu kutoka mita 90 hadi mita 300 na lina joto la wastani wa sentigradi 270 na mvua ya milimita 350 hadi milimita 700 kila mwaka. Shughuli kuu ndani ya eneo hili ni ufugaji na wanyamapori.



*Vijabiz Dairy Value Chain-Kilifi County*



***Eneo la minazi, mikorosho na Mihogo:*** Eneo hili hupatikana hasa katika maeneo bunge ya Kilifi Kusini na Kaskazini na ndio eneo dogo zaidi ya maeneo yote. Liko kwenye mwinuko wa kati ya mita 30 hadi mita 310 juu ya usawa wa bahari na joto la wastani wa sentigredi 270 na mvua ya milimita 900 kila mwaka.Eneo hilo lina uwezo sawa wa mazao yanayopatikana katika maeneo ya minazi-mihogo na mikorosho- mihogo.

## 1.3Vitengo vya Utawala na Siasa

### *1.3.1 Vitengo vya Utawala*

Kuna kaunti ndogo 7, tarafa 18, lokesheni 61 na lokesheni ndogo182. Zote hizi zapatikan ndani ya eneo la kilomita mraba 12178. Kaunti ndogo ya Magarini ndiyo kubwa zaidi yenye eneo la kilomita mraba 5229 ilhali Rabai ikiwa ndio kaunti ndogo zaidi inayochukua eneo la kilomita mraba 208.
Kuna wadi 18 za usimamizi na uchaguzi za serikali ya kaunti na vijiji 1,912 katika kaunti hii. Habari hii imefupishwa katika Jedwali 1.1. Pia Kaunti ndogo za Kaunti ya Kilifi zenye tarafa, lokesheni na lokesheni ndogo pamoja na ukubwa zimewasilishwa katika Jedwali 1.1.

Jedwali 1.1: Maeneo kwa kilomita mraba ya kaunti ndogo

| Kaunti ndogo | Idadi ya tarafa | Idadi ya lokesheni | Idadi ya lokeseni ndogo | Eneo kwa kilomita mraba |
|---|---|---|---|---|
| Kilifi kaskazini | 1 | 5 | 14 | 264 |
| Kilifi kusini | 1 | 3 | 11 | 291 |
| Malindi | 2 | 8 | 31 | 2,263 |
| Kaloleni | 3 | 8 | 20 | 706 |
| Magarini | 2 | 9 | 27 | 5,229 |
| Ganze | 4 | 14 | 45 | 3,218 |
| Kauma | 1 | 3 | 9 | 181 |
| Chonyi | 1 | 4 | 9 | 193 |
| Rabai | 3 | 7 | 16 | 208 |
| Jumla | **18** | **61** | **182** | **12,553** |

*Chanzo: KNBS, Sensa ya 2019*

## 1.4 Vipengee vya Idadi ya Watu

### *1.4.1Idadi ya Watu, Mchanganyiko na Maenezi*

**Muundo wa Umri wa Idadi ya Watu katika Kaunti**

Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi nchini Kenya ya mwaka 2019, Kaunti ya Kilifi ilikuwa na jumla ya wakazi 1,453,787 wanaume 704,089 na wanawake 655,673 (Angalia Jedwali 1.2). Kaunti hii ina ukubwa wa idadi ya watu katika kila nyumba ya wastani wa 4.8. Malindi ndiyo kaunti ndogo yenye watu wengi zaidi ilhali Chonyi na Kauma zikiwa na idadi ndogo zaidi ya wakaazi.Kufikia mwisho wa 2022, idadi ya wanaume ilipungua hali ile ya wanawake ikaongezeka. Idadi ya wanawake ilikuwa chini kuliko idadi ya wanaume mnamo 2019, makadirio ya 2022, 2025 na 2027 yanaonyesha idadi kubwa ya wanawake katika kaunti zote ndogo na hatimaye katika kaunti nzima.

Jedwali1.2: Makadirio ya idadi ya watu kijinsia kwa kila kaunti ndogo

| kaunti | Sensa ya 2019 | | | | 2022(Makadirio) | | | 2025(Makadirio) | | | 2027(Makadirio) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Watu wa jinsia tofauti | Jumla | Wanaume | wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kilifi | 704,089 | 749,673 | 25 | 1,453,787 | 769,120 | 778,627 | 1,547,747 | 813,735 | 822,775 | 1,636,510 | 843,651 | 852,575 | 1,696,226 |
| Chonyi | 29,527 | 32,807 | 1 | 62,335 | 32,254 | 34,074 | 66,364 | 34,125 | 36,006 | 70,170 | 35,380 | 37,310 | 72,730 |
| Ganze | 66,921 | 76,981 | 4 | 143,906 | 73,102 | 79,954 | 153,207 | 77,342 | 84,488 | 161,993 | 80,186 | 87,548 | 167,904 |
| Kaloleni | 92,614 | 101,063 | 3 | 193,682 | 101,168 | 104,966 | 206,200 | 107,037 | 110,918 | 218,025 | 110,972 | 114,935 | 225,981 |
| Kauma | 10,965 | 11,673 | 0 | 22,638 | 11,978 | 12,124 | 24,101 | 12,673 | 12,811 | 25,483 | 13,138 | 13,275 | 26,413 |
| Kilifi Kaskazini | 86,986 | 91,836 | 2 | 178,824 | 95,020 | 95,383 | 190,382 | 100,532 | 100,791 | 201,300 | 104,228 | 104,442 | 208,645 |
| Kilifi kusini | 101,852 | 104,897 | 4 | 206,753 | 111,259 | 108,948 | 220,116 | 117,713 | 115,126 | 232,739 | 122,041 | 119,295 | 241,232 |
| Magarini | 93,302 | 98,308 | 2 | 191,610 | 101,920 | 102,105 | 203,994 | 107,832 | 107,894 | 215,693 | 111,796 | 111,802 | 223,564 |
| Malindi | 163,351 | 169,866 | 9 | 333,226 | 178,438 | 176,427 | 354,763 | 188,789 | 186,430 | 375,108 | 195,730 | 193,182 | 388,796 |
| Rabai | 58,571 | 62,242 | 0 | 120,813 | 63,981 | 64,646 | 128,621 | 67,692 | 68,311 | 135,998 | 70,181 | 70,785 | 140,960 |

*Chanzo: KNBS, 2019*

Kaunti ndogo yenye watu wengi zaidi katika Kaunti ya Kilifi ni Malindi yenye wakazi 333,226 ikifuatwa na kaunti ndogo za Kaloleni, Magarini na Kauma zenye wakazi 193,682, 191,610 na 22,638 mtawalia. Idadi ya wanawake katika Kaunti ya Kilifi ni kubwa kuliko idadi ya wanaume katika kaunti zote ndogo na kuna pia watu wa jinsia tofauti 25.

Kidokezo: Watu 17 hawakutaja umri wao (wanaume 6 na wanawake 11) lakini wamo katika jumla zao.

### *1.4.2 Msongamano wa Watu na Maenezi*

Kaunti ya Kilifi ina jumla ya wakazi 1,453,787. Idadi ya watu kwa sasa inakadiriwa kuwa 1,517824 na inakadiriwa kuwa 1,686,705 na 1,858,772 ifikapo 2025 na 2027 mtawalia. Hivi sasa, wamesongamana watu 116 kwa kila kilomita mramba ambayo inakadiriwa kuongezeka hadi watu 148 kwa kila kilomita mraba ifikapo 2027.

Kaunti ndogo iliyo na watu wengi zaidi ni Kilifi Kusini yenye watu 713 kwa kila kilomita mraba huku Magarini na Ganze zikiwa na watu 37 na 45 kwa kila kilomita mraba mtawalia. Katika kipindi cha miaka mitano, Kilifi Kusini na Kilifi Kaskazini zimesalia kuwa na watu wengi zaidi huku Magarini na Ganze zikisalia kuwa na idadi ndogo ya watu. Msongamano wa watu kwa kaunti ndogo tofauti za Kilifi umewasilishwa katika Jedwali 1.3.

**Jedwali 1.3: Usambazaji na wingi wa watu kulingana na kaunti ndogo**

| Kaunti ndogo | Sensa ya 2019 | | | 2022 (Makadirio) | | | 2025 (Makadirio) | | 2027 (Makadirio) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Eneo kwa kilomita mraba | Idadi ya watu | Msongamano wa watu | Eneo kwa kilomita mraba | Idadi ya watn | Msongamano wa watu | Idadi ya watu | Msongamano wa watu | Idadi ya watu | Msongamano wa watu |
| Kilifi Kaskazini | 264 | 178,824 | 677 | 264 | 190,382 | 721 | 201,300 | 763 | 208,645 | 790 |
| Kilifi kusini | 290 | 206,753 | 713 | 290 | 220,116 | 759 | 232,739 | 802 | 241,232 | 832 |
| Malindi | 2,263 | 333,226 | 147 | 2263 | 354,763 | 157 | 375,108 | 166 | 388,796 | 172 |
| Kaloleni | 706 | 193,682 | 274 | 706 | 206,200 | 292 | 218,025 | 309 | 225,981 | 320 |
| Magarini | 5,229 | 191,610 | 37 | 5,229 | 203,994 | 39 | 215,693 | 41 | 223,564 | 43 |
| Ganze | 3,218 | 143,906 | 129 | 3218 | 153,207 | 48 | 161,993 | 50 | 167,904 | 52 |
| Kauma | 181 | 22,638 | 125 | 181 | 24,101 | 133 | 25,483 | 181 | 26,413 | 146 |
| Chonyi | 193 | 62,335 | 323 | 193 | 66,364 | 344 | 70,170 | 364 | 72,730 | 377 |
| Rabai | 208 | 120,813 | 581 | 208 | 128,621 | 618 | 135,998 | 654 | 140,960 | 678 |

*Chanzo: KNBS, 2019*

Kaunti ndogo ya Kilifi Kusini ina msongamano mkubwa zaidi wa watu (watu 713 kwa kila kilomita mraba) ikifuatiwa na Kilifi Kaskazini (watu 677 kwa kila kilomita mraba) kisha Magarini (watu 37 kwa kila kilomita ya mraba).

### *1.4.3 Hali ya Umaskini*

Kiwango cha umaskini wa kifedha katika kaunti ya Kilifi ni asilimia 46.1 ambayo ni asilimia 10 zaidi ya kiwango cha kitaifa cha asilimia 35.7 huku takriban watu 670,448 huko Kilifi wakiwa maskini wa kifedha. Kilifi ina kiwango cha umaskini wa viwango tofauti cha asilimia 59.9, ambacho ni asilimia 12 zaidi ya kiwango cha umaskini wa aslilmia 47.7 huku jumla ya watu 870,425 wakiwa maskini wa viwango tofauti.

Kielelezo 1.2: hali ya umaskini katika kaunti ya Kilifi

Inapogawanywa kwa vikundi kwa umri, asilimia 57.1 ya watoto katika kaunti Kilifi ni masikini wa viwango vingi (kielelezo 1.2). Hii ni pointi 5 zaidi ya wastani wa kitaifa wa asilimia 52.5. Miongoni mwa vijana, asilimia 61.8 ni maskini wa viwango vingi ikilinganishwa na wastani wa kitaifa wa asilimia 48. idadi ya wazee maskini wa viwango vingi ni asilimia 64.2 ikilinganishwa na wastani wa kitaifa wa asilimia 55.7.

Kielelezo 1.2: hali ya umaskini katika kaunti ya Kilifi






# Uhakiki wa Utendaji wa Kaunti 2018-2022

# 2



## 2.1 Uhakiki wa Utendaji wa CIDP II (2017-2022)

Uchanganuzi wa vyanzo vya mapato vya kaunti kulingana na makadirio na mapato halisi umewasilishwa katika Jedwali 2.1 na kielelezo 2.1.

### Jedwali 2.1: Uchanganuzi wa vyanzo vya mapato vya kaunti

| Chanzo cha mapato | Makadirio ya mapato (Ksh. milioni) | | | | | Mapato halisi (Ksh. milioni) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | FY1 | FY 2 | FY3 | FY 4 | FY 5 | FY1 | FY2 | FY3 | FY4 | FY5 |
| a) mgawo sawa/ kutoka serikali kuu | 9,950.90 | 10,833.00 | 11,077.11 | 10,444.50 | 11,641.59 | 9,950.90 | 10,833.00 | 11,077.11 | 10,444.50 | 6,246.41 |
| b) Ruzuku za masharti (GoK) | 911.00 | 564.23 | 513.22 | 554.01 | - | 550.70 | 793.07 | 331.31 | - | 473.64 |
| c) Ruzuku za masharti (washirika wa maendeleo) | 262.60 | 1,130.33 | 1,500.52 | 1,253.23 | - | 114.67 | 261.96 | 906.33 | - | - |
| d) Mapato ya kaunti | 929.66 | 1,400.00 | | 1,150.00 | 925.00 | 522.33 | 864.32 | 793.71 | 829.72 | 433.39 |
| e) Vyanzo vingine (taja) | | | | | | | | | | |
| **Jumla** | **12,054.16** | **13,927.56** | **13,090.85** | **13,401.74** | **12,566.59** | **11,138.60** | **12,752.35** | **13,997.59** | **11,274.22** | **7,524.14** |

### Kielelezo 2.1: Uchanagnuzi wa Mapato ya Kaunti Dhidi ya Mapato Yanayotokana na Serikali Kuu



## 2.2 Uhakiki wa Matumizi ya Kaunti

Kwa wastani, kaunti ilitumia asilimia 72 ya bajeti iliyotengwa huku sekta ya barabara ikiwa na viwango vya juu zaidi vya utumiaji (Jedwali 2.2). Hili linathibitishwa na idadi kubwa ya barabara zilizowekwa lami katika Kaunti.

**Jedwali 2.2: Uchanganuzi wa Matumizi ya Kaunti**

| Idara | Jumla ya mgawo wa bajeti (Milioni KES) | Jumla ya matumizi halisi(Milioni KES) | Tofauti(Milioni KES) | Viwango vya matumizi |
|---|---|---|---|---|
| Bunge la Kauniti | 5,206.36 | 4,254.33 | 952.03 | 82% |
| Halmashauri Kuu ya Kaunti | 2,586.28 | 1,890.37 | 695.91 | 73% |
| Fedha na mipango ya uchumi | 4,037.79 | 2,563.69 | 1,474.10 | 63% |
| Kilimo Mifugo na Uvuvi | 4,327.05 | 3,185.54 | 1,141.51 | 74% |
| Maji na mazingira | 7,510.49 | 5,930.90 | 1,579.59 | 79% |
| Elimu na teknolojia | 6,906.31 | 4,956.58 | 1,949.73 | 72% |
| Huduma za afya za kaunti | 17,739.75 | 12,669.25 | 5,070.50 | 71% |
| Barabara, Uchukuzi na Kazi za umma | 8,274.10 | 7,677.11 | 596.99 | 93% |
| Ardhi, Nishati na mipango tekelezi | 3,353.69 | 2,366.29 | 987.40 | 71% |
| Teknolojia, huduma za serikali mtandaoni na huduma za jamii | 250.56 | 137.85 | 112.71 | 55% |
| Biashara, utalii na maendeleo ya vyama vya ushirika | 1,710.35 | 1,365.35 | 345.00 | 80% |
| Bodi ya watumishi wa umma ya Kaunti | 375.72 | 238.80 | 136.92 | 64% |
| Ugatuzi, usimamizi wa Maafa na Utumishi wa Umma | 11,493.11 | 6,216.73 | 5,276.38 | 54% |
| **Jumla** | **73,771.56** | **53,452.79** | **20,318.77** | **72%** |

Uchanganuzi wa matumizi halisi yamewasilishwa kwenye kielelezo 2.2. Inaonyesha kuwa huduma za afya zilikuwa na mgao wa juu zaidi na matumizi pia.

**kielelezo 2.2: Uchanganuzi wa Matumizi ya Bajeti Kisekta**




## 2.3 Uhakiki wa Utendaji wa Sekta Tofauti

Wakati wakutekeleza CIDP II (2017-2022) mafanikio kadhaa yalipatikana. Baadhi ya mafanikio muhimu kwa kila sekta yamewasilishwa katika sehemu zifuatazo:

### 2.3.1 Sekta ya Afya

**Mafanikio Muhimu Wakati wa Kipindi cha CIDP II (2018-2023)**



*Kituo cha  Matibabu Katika Kaunti ya  Kilifi*

***Ili kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, yafuatayo yalitimizwa***

- *Idadi ya wanawake waliofanya angalau ziara 4 kuhudhuria kliniki ya uzazi (ANC) iliongezeka kutoka aslilimia 32 hadi aslilimia 57. Matumizi ya Uongezaji wa Asidi ya Foliki ya madini ya chuma (IFAS) kati ya akina mama wajawazito yaliongezeka kutoka asilimia 72 hadi asilimia 89*
- *Uzalishaji uliofanywa na wakunga wenye ujuzi uliimarika kutoka asilimia 53 hadi asilimia.*
- *Mimba za utotoni zimepungua kutoka asilimia 26 hadi asilimia 14 dhidi ya lengo la asilimia17.*



- *Huduma ya watoto wachanga chini ya mwaka 1 waliopatiwa chanjo kamili iliongezeka kutoka asilimia 67 hadi asilimia 78 huku idadi ya watoto wachanga walio na uzito mdogo wa kuzaliwa iliongezeka kutoka asilimia 6.7 hadi asilimia 9.*
- *Kiwango cha uongezaji wa vitamini A miongoni mwa watoto wa miezi 12-59 kiliongezeka kutoka asilimia 69 hadi asilimia100 huku upatikanaji wa dawa za minyoo kwa kundi la umri huo huo uliongezeka kutoka asilimia 23 hadi asilimia 100 kutokana na matokeo ya programu inayofanyika mara mbili kwa mwaka ya Malezi Bora ambayo utenda kazi wake uliongezwa.*
- *Maambukizi ya ukimwi yalipungua kutoka asilimia 4.2 hadi asilimia 3.5 kutokana na hatua zilizowekwa katika utambuzi,ubainishaji, kuanzisha na kuendelea na matibabu.*
- *Idadi ya waliogunduliwa na malaria miongoni mwa raia ilipungua kutoka asilimia 7.2 hadi asilimia 4.7 dhidi ya lengo la asilimia 2 kutokana na kuongezeka kwa hatua za kuzuia malaria.*
- *Kiwango cha vifo vya kutokana na Kifua Kikuu kiliongezeka kutoka asilimia 8 hadi asilimia 11 dhidi ya lengo la asilimia 3 hali hii ilihusishwa na kupungua kwa uchunguzi na ufuatiliaji wa mara kwa mara.*






*Kitengo cha Vitanda 3 vya wagonjwa wa figo katika Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Kilifi*

**Kuongeza ufikiaji wa huduma maalum:**

- *Kitengo cha wagonjwa mahututi (ICU), kumbi za uendeshaji upasuwaji, wadi za jumla, wadi za kibinafsi na za ajali na dharura katika kituo cha matibabu cha Kaunti ya Kilifi; kitengo cha usafishaji damu kwa mashine ya figo; kituo kimoja tegemezi cha kuongezewa damu katika Hospitali ndogo ya kaunti iliyoko Malindi kilianzishwa na kufanya kazi.*
- *Idadi ya hospitali za umma zinazotoa huduma kwa wagonjwa waliolazwa iliongezeka kutoka 5 hadi 9, zile zinazotoa huduma za maabara ya msingi ziliongezeka kutoka 57 hadi 102 ilhali vituo vya umma 4 vya ngazi ya 3 vilipandishwa hadhi hadi ngazi ya 4.*



### 2.3.2 Sekta ya Elimu

***Ili kuboresha upatikanaji wa Elimu Bora ya Maendeleo ya utotoni, yafuatayo yalitekelezwa***

- *Jumla ya uandikishaji wa wanafunzi wa maendeleo ya elimu ya utotoni (ECD) iliongezeka kwa kiwngo kutoka asilimia 95.8 mwaka 2018 hadi asilimia 96.2 2022 dhidi ya lengo la asilimia 97.5*
- *Kiwango cha watoto kutoka kiwango kimoja hadi kinginekiliongezeka kutoka asilimia 45 hadi asilimia 90 dhidi ya lengo la asilimia 70.*
- *Kiwango cha watoto kubakia shule kiliongezeka kutoka asilimia 63 hadi asilimia 87 dhidi ya lengo la asilimia 88.*
- *Uwiano wa mwalimu - mwanafunzi uliongezeka kutoka 1:204 mwanzoni mwa kipindi cha mpango hadi 1:37 dhidi ya lengo la 1:45.*
- *Hii ilichangiwa na ujenzi wa vyumba vya madarasa 785, kuajiriwa kwa walimu 1,284 wa shule za maendeleo ya awali ya watoto na utoaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa shule zote za awali za umma za kaunti*



**785**

Idadi ya madarasa mapya

*Shule ya awali ya Tsakalorovu katika wadi ya Kaloleni*




***Ili Kuongeza Upatikanaji wa Elimu katika vituo vya mafunzo ya ufundi, yafuatayo yalitekelezwa***

- *Usajili katika vituo vya mafunzo ya ufundi uliongezeka kutoka wanafunzi 3,291 mwanzoni mwa kipindi cha mpango hadi 7,600 wakati wa kufunga kipindi cha mpango dhidi ya lengo la 5,300.*
- *Kiwango cha ukamilishaji masomo katika vituo vya mafunzo ya ufundi kiliongezeka kutoka asilimia 37 hadi asilimia 80 dhidi ya lengo la asilimia 87.*
- *Haya yametokana na ujenzi madarasa 96 ambayo yalikamilika ilhali 43 yakiendelea katika wadi 35 na kuongezeka kwa kampeni za utangazaji na uhamasishaji.*
- *Idadi ya vituo vya mafunzo ya ufundi vinavyotoa mtaala wa teknolojia TEHAMA iliongezeka kutoka vituo 34 hadi 38 huku vituo 36 vikiwa na zana na vifaa vya kisasa kutoka 24 vilivyokuwa na vifaa awali.*

### 2.3.3 Uhifadhi wa Mazingira, Maji, Usafi wa Mazingira na Maliasili

*Katika Katika kipindi cha uhakiki, nyumba zilizo na maji safi ziliongezeka kutoka asilimia 50 hadi asilimia 70 dhidi ya lengo la asilimia 90.*

- *Uchimbaji na ukarabati wa visima 40 na 41 mtawalia.*
- *Kuweka pampu 16 zinazotumia nishati ya jua sambamba na ujenzi wa mabwawa 3, sufuria 5 za maji na visima 8 vya vina vifupi.*
- *Jumla ya mabomba ya maji yenye urefu wa Km 23.5 yalifanyiwa ukarabati na mabomba mapya yenye urefu wa Km 331.4 yalitandazwa; Vibanda 189 vilijengwa na matangi 90 ya maji yaliwekwa.*



***Ili kuimarisha usafi wa mazingira, sekta hii ilichukua hatua zifuatazo:***

- Imetengewa ekari 14 za ardhi kwa ajili ya kituo cha kutibu tope/taka (ekari 4 Mtwapa, ekari 2 Mtondia, ekari 4 Watamu na ekari 4 Malindi) pamoja na kununua “vinyonyaji vya asali” Nne ④.

- Asilimia 52 ya watu walihamasishwa kuhusu usimamizi wa taka dhidi ya lengo la asilimia 38 kati ya 2017 na 2022, ufuataji wa miongozo ya mazingira ilipanda kutoka asilimia 55 hadi asilimia 63 katika kipindi hicho.

- Kuweka asilimia 15 ya mashamba chini ya miti ya mbao dhidi ya lengo la asilimia 36; uanzishaji wa bustani ya kaunti ya miche ambayo ilisambaza miche ya miti bure kwa wakulima; Kupanda miti ya mikoko; mpango wa “shule za kijani”; uundaji wa Sheria mbili yaani Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu ya Kaunti ya Kilifi, 2019 pamoja na Sheria ya Mazingira ya Kaunti ya Kilifi (taratibu na Udhibiti), 2016. Sera moja pia ilitengenezwa; Sera ya Misitu ya Kaunti ya Kilifi, 2016. Zaidi ya hayo, Hekta 500 za ardhi iliyoharibiwa ilirekebishwa dhidi ya lengo la Hekta 640.

- Kuanzishwa kwa Sheria ya Hali ya Hewa ya Kaunti ya Kilifi. Aidha, mikutano 80 ya uhamasishaji juu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ilifanyika dhidi ya lengo la mikutano140.

- Idadi ya nyumba zilizo kubali kuishi maisha ya uelewa mzuri wa hali ya hewa katika kipindi cha uhakiki iliongezeka kutoka asilimia 38 hadi asilimia 40.

- Utumiaji wa teknolojia ya mabadiliko ya tabianchi inayotilia maanani mahitaji ya Kilifi uliboreshwa hadi asilimia 53 dhidi ya lengo la asilimia 60.

- Hii ilitokana na utendakazi wa Sheria ya Mabadiliko ya Tabianchi ya Kaunti ya Kilifi, 2021; utengaji wa asilimia 0.5 ya bajeti ya maendeleo kwa hatua za mabadiliko ya tabianchi; na kujenga uelewa juu ya mabadiliko ya tabianchi kupitia ushirikiano.



*Msitu wa Jamii wa Mikoko Kilifi*

### 2.3.4 Utawala wa Umma na Mahusiano ya Kiserikali

- *Ili kuboresha mipango ya kiuchumi na uratibu wa sera, sekta ilitayarisha nyaraka kadhaa za kisheria kwa wakati. Yaani ADP, APR, CFSP na CBROP, pia, Sekta ilitengeneza kijitabu cha Viashirio na rasimu ya sera ya M & E.*
- *Ili kukuza usimamizi mzuri wa fedha za umma, Kaunti ilitayarisha makadirio ya Bajeti kwa wakati unaofaa (PBB) kwa kufuata CFSP, kaunti iliwasilisha ripoti za kifedha na ukaguzi kulingana na mahitaji ya kisheria. Hii iliwezesha kaunti kudumisha maoni ya ukaguziyenye sifa zinazostahili.*
- *Mapato ya vyanzo vya kaunti yenyewe yaliongezeka kwa asilimia 0.2*
- *Kuhusu utendakazi wa matumizi, kaunti ilitumia Kshs. 53.5 bilioni dhidi ya Kshs. bilioni 73.8 katika kipindi cha mpango huo. Inaonyesha kiwango cha matumizi cha asilimia 72. Hii ilitokana na kuchelewa kutolewa kwa hazina kutoka wizara ya fedha na mapungufu katika ukusanyaji wa mapato ya kaunti yenyewe.*
- *Ili kuimarisha ushiriki wa umma na elimu ya raia, Kaunti ilitunga sera ya ushiriki wa umma na kuandaa Mswada wa Ushiriki wa Umma. Kaunti iliendelea kuwashirikisha wananchi wake katika masuala yote yanayowahusu kupitia vikao vya ushirikishwaji wa umma.*
- *Ili kuboresha utoaji wa huduma, sekta iliweka maafisa wakuu wa kaunti (CECMs, Cos na Wakurugenzi) chini ya kandarasi ya utendakazi na wafanyikazi wote wa kaunti waliwekwa chini ya mfumo wa kutathmini utendakazi.*
- *Ili kutoa huduma kwa ufanisi, sekta ilianzisha ofisi 35 za wasimamizi wa wadi. Hili lililenga kusogeza huduma karibu na wananchi.*

### 2.3.5 Sekta ya Ulinzi wa Jamii, Utamadunu na Burudani

- *Kesi zilizoripotiwa za mimba za watoto zilipungua kutoka 156 hadi 112. Hii ilitokana na mijadala kuhusu Afya ya Uzazi wa Kijamii kwa Vijana (AYSRH) ambayo ilibadilisha tabia ya vijana.*
- *Ilisambaza vifurushi 3,000 vya kuwazidishia hadhi watoto wanaoenda shule na kuandaa Sera ya Ulinzi wa Mtoto ya Kaunti ya Kilifi.*
- *Watoto 200 waliohamasishwa kwenye stadi za maisha ili kufanya maamuzi bora na sahihi na pia kukua na kuwa watu wazima wanaowajibika.*
- *Ili kukamilisha uhamishaji wa pesa kwa wazee, serikali ya Kaunti ilihamisha Ksh. milioni 29 kila mwaka kwa wanufaika 1,029 katika kipindi cha cha uhakiki.*
- *Kaunti ilitoa mafunzo kwa wanawake 2,000 kuhusu ujuzi wa uwekezaji au ujasiriamali na kufanya vikao 140 vya uhamasishaji kuhusu ukatili wa kijinsia(GBV). Kutokana na haya, kulikuwa na ongezeko la idadi ya kesi za ukatili wa kijinsia zilizoripotiwa kutoka kesi 700 mwaka 2021 hadi zaidi ya kesi 1,000 mwaka 2022.*
- *Kaunti ilitoa ushauri kwa vijana 5,000 katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya kibinafsi, ilisaidia katika uundaji na uelimishaji wa vikundi 2,500 vya vijana na kuona vijana 25,000 wakishiriki katika uwajibikaji wa kiraia. Kutokana na vikao vya uhamasishaji vilivyofanyika, vijana 3,000 walipata ufadhili chini ya YEDF, WEF na UWEZO huku vijana 3,000 wakinufaika na AGPO.*
- *Ilikarabati vituo 18 vya michezo dhidi ya lengo la 23, ilisambaza vifaa na zana za michezo kwa timu 385 dhidi ya lengo la timu 285.*
- *Ilitoa mafunzo kwa marefa 20, makocha 20 na wasaidizi wa huduma ya kwanza 20 dhidi ya lengo la wanamichezo 50.*



*Jumba la Sanaa la Chonyi*

### 2.3.6 Agriculture, Livestock Development and Fisheries

- *Maize production per acre increased from 3bags to 14 bags, cassava from 3-5tonnes to 20 tonnes per acre. This increase could be attributed to several interventions implemented by the county.*
- *Supplied subsidized inputs for improved and certified crop varieties amounting to 256 tonnes of seed and 190,866 seedlings, 279,674 farmers trained on good agricultural practices including climate smart agriculture, 1142Ha under irrigation farming as well as adoption of mechanization.*
- *There was an increase in Hectarage in land under crop production from 528 to 865 over the planning period.*
- *Recruited 45 new extension staff which improved extension service delivery.*
- *In livestock production, there was 46 percent increase in milk production from 6,335,156 litres of milk to 11,020,977 litres of milk due to improved dairy breeds as a result of scaled up provision of Artificial insemination services.*
- *A total of 16,409 inseminations were carried out in the county and 729 dairy cattle were procured and distributed to the farmers' county wide.*
- *A total of 15,000 goats and sheep processed and exported through Ngomeni port to Oman and middle east, and 30 hybrid galla goats from ADC Galana and Kisiwani were processed and exported to Bujumbura in Burundi.*
- *There was 50 percent Increase in vaccinations activities with 2,055,522 animals reached with vaccines in the county.*
- *Established 5 livestock sale yards in the county thus leading to improved income for the farmers. Chevon and mutton production in the county increased by 39 percent due to procurement and distribution of 1,819 hybrid galla goats to farmers for breed improvement.*
- *Fish tonnage in aquaculture increased from 2,697kg to 3,171kgs annual production. This was attributed to the rehabilitation of 94 fish ponds and establishment 3 aquaculture hatcheries.*
- *283 fishermen were provided with fishing gears; 5 fish landing facilities and 890 fish traders/BMUs members were trained on fish handling; quality and safety issues; 4 functional fisherman cooperative societies established; 4 functional policies and legislation were developed; and 4 spatial plans for fishing grounds were developed. societies were established.*

### 2.3.7Ardhi, Nyumba, Mipango Tekelezina Maendeleo ya Miji

- *Kufungua na kuboresha kilomita 40 za barabara za kuingia katika miradi ya makazi dhidi ya lengo la kilomita 100; na kuanzisha mradi wa nyumba za kununuliwa polepole wa Kaunti wa jumla ya KShs.120 milioni.*
- *Kutayarisha na kuidhinisha mpango wa kianga wa kaunti; ilitayarisha mipango 30 ya vituo vya miji kati ya hiyo 4 iliidhinishwa; na kuanzisha manispaa 2 ndani ya kaunti dhidi ya lengo la 5.*
- *Kupimwa na kukadiria thamani ya ardhi Hekta 22,997; kuwezesha ugawaji wa viwanja 24,130; kupima na kukamilisha skimu 6 za makazi na sehemu zilizoamuliwa; Wezesha utoaji wa hati miliki za ardhi kwa taasisi 78 za umma na kupima vituo 10 vya mijini na biashara.*
- *Ili kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya mali ya umma, sekta ilitengeneza na kutekeleza orodha ya uthamini wa Kaunti nzima na kutoa ripoti ya thamani ya mali ya kaunti.*
- *Ilianzisha na kufanya kazi maabara ya GIS; na kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Ardhi.*

*Kaunti ilitayarisha mipango 30 ya vituo vya miji kati ya hiyo 4 iliidhinishwa*



Taa la mlingoti wa juu katika mji mdogo wa Tezo



Barabara za viungo Kilifi

### 2.3.8 Sekta ya Nishati na Miundo Msingi

- *Idadi ya nyumba zilizounganishwa kwenye gridi ya umeme iliongezeka kutoka asilimia 21 hadi asilimia 64*
- *Zaidi ya taa 200 za barabarani na taa100 za milingoti ya juu zaidi ziliwekwa;*
- *Uwiano wa umeme unaozalishwa kutoka vyanzo vya nishati mbadala vilivyogawanywa kwa aina na matumizi (MW) uliongezeka kutoka 3MW hadi 44MW. Hii ni kutokana na kuanzishwa kwa mtambo wa kuzalisha umeme wa jua wa 40MW katika kaunti na pia Gongoni salt ltd ambayo ilitengeneza mitambo miwili ya umeme wa jua yenye uwezo wa 0.5MW kila moja kwa matumizi viwanda vyao;*
- *Idadi ya nyumba zinazotumia majiko ya kuokoa nishati na teknolojia zinazohusiana iliongezeka kutoka 50 hadi 3,000;*
- *Kaunti iliweka lami kilomita 50 za barabara, iliboresha, kukarabati na kudumisha barabara kilomita 1,556 dhidi ya lengo la kilomita 2,500;*
- *Madaraja ya miguu10 yalidumishwa/kukarabati; kilomita 8 za mifereji ya maji ya dhoruba ilikarabatiwa dhidi ya lengo la kilomita 20; na*
- *Kupanua viwanja 2 vya mabasi vilivyopo na kujenga viwanja 2 vipya vya mabasi na kuweka taa 200 za barabarani na mataa mengi.*

### 2.3.9Maendeleo ya Biashara, Utalii, Viwanda na Makundi ya Ushirika

- *Kujenga masoko mapya 17 na kukarabati masoko 5, kujengea masoko 6 ukuta, kujenga vituo 16 vya usafi, na kuchimba visima 2;*
- *Ilitoa Kshs 321,000,000 kwa vikundi 2,426 na vyama vya ushirika 34 kupitia Mfuko wa Fedha wa biashara ndogo wa Kaunti ya Kilifi;*
- *Katika uhamasishaji wa uwekezaji, kaunti ilitengeneza maelezo mafupi manne ya kisekta na miradi 12 ya uwekezaji kibenki;*
- *Kitengo cha mizani na vipimo cha Kaunti kilirekebisha mashine 8,730 za kupimia, kikukagua majengo 390 ya biashara na kuunda viwango na zana za kufanya kazi;*
- *Banda la wageni la mlango wa mto Sabaki lilijengwa; kushiriki katika Kampeni 6 za Kusafisha Ufuo; ilifanya matangazo 8 kwenye vyombo vya habari; na kuandaa tamasha 3 za utalii wa Utamaduni na matukio 10 ya utalii wa michezo; na*
- *Wasimamizi 200 wa ufuo wa bahari na vikundi 4 vya kijamii vya utalii wa kiikolojia pia walipewa mafunzo.*
- *Ili kuiuza Kilifi kama kivutio cha watalii sekta hii pia ilishiriki katika maonyesho ya hadhara ya utalii ya ndani na nje ya nchi na kuwezesha uuzaji wa maeneo lengwa kupitia jukwaa la masoko ya kidijitali 'This is Kilifi'*
- *Ili kuboresha miundomsingi ya utalii, sekta iliwezesha ujenzi wa ukuta wa soko la Utalii la Watamu, nyumba ya walinzi na nyumba ya kutawadha.*
- *Vyama vipya 54 vya ushirika vilisajiliwa, ukaguzi wa kisheria wa vyama vya ushirika 334 na ukaguzi wa vyama vya ushirika 66 na ukaguzi wa hapo kwa hapo ulikamilika.*
- *Jumla ya siku za elimisha wanachama 65 na warsha 72 za kamati za viongozi wa vyama vya ushirika pia zilifanyika.*



Soko la Oloitiptip



## 2.4 Changamoto za Utekelezaji wa CIDP II

Kaunti ilikabiliwa na changamoto zifuatazo wakati wa utekelezaji wa CIDP II:

i. Upungufu wa mgao wa bajeti na ucheleweshaji wa kutolewa kwa hazina kutoka kwa wizara ya fedha kwa utekelezaji wa miradi na programu nyingi;
ii. Upungufu wa watu wenye ujuzi wa kiufundi katika sekta nyingi;
iii. Upungufu wa takwimu za kutayarisha sera, upangaji, ufuatiliaji na utathmini;
iv. Kubadilika kwa mambo yaliyopewa kipaumbele na wafadhili kutokana na majanga ya kimataifa;
v. Kupungua kwa ufadhili kulisababisha matatizo katika bajeti ya idara hasa katika ufadhili wa huduma ya afya ya msingi;
vi.
vii. Ukosefu wa mfumo mzuri wa kuratibu washirika na wadau katika sekta mbalimbali; na
viii. Masuala yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi kama vile mafuriko na ukame

## 2.5 Masuala Ibuka Katika Utekelezaji wa CIDP II

Yafuatayo ni masuala yaliyojitokeza katika kipindi cha utathmini:

i. Janga kubwa la covid-19;
ii. Wadudu na magonjwa ibuka; na
iii. Mabadiliko ya sera hasa kutoza VAT kwenye mashini ya kilimo.

## 2.6 Mafunzo Kutoka kwa Utekelezaji wa CIDP II

Yafuatayo ni mafunzo tuliyojifunza wakati wa utekelezaji wa CIDP iliyopita:

i. Mikakati ya uhamasishaji wa rasilimali unaweza kuongeza, kusaidia na kuendeleza utekelezaji wa programu;
ii. Ushiriki wa mapema wa bunge la kaunti katika uundaji wa sera na upangaji ni muhimu;
iii. Mifumo ya ufuatiliaji na tathminim (M&E) na takwimu iliyoratibiwa vyema ni muhimu kwa utekelezaji wa CIDP
iv. Uendeshaji wa huduma kwa kutumia teknolojia unaweza kuboresha utoaji wa huduma;
v. Upangaji unaotilia maanani taarifa za kutarajia/hatari ni muhimu;
vi. Mbinu ya kuhusisha wadau mbalimbali katika utekelezaji wa programu ni muhimu; na
vii. Ushirikiano wa sekta ya umma na sekta za kibinafsi unaweza kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali mikubwa.

## 2.7 Ukadiriaji wa Maliasili za Kaunti

Jedwali 2.3linawasilisha rasilimali za kaunti na sekta tegemezi pamoja na fursa na vikwazo vya matumizi bora.

**Jedwali 2.3: Tathmini ya maliasili**

| Maliasili | Sekta tegemezi | Hali, kiwango cha matumizi, mtizamo wa siku zijazo | Fursa za matumizi bora | Vikwazo vya matumizi bora | Mikakati iliyopo ya usimamizi endelevu |
|---|---|---|---|---|---|
| Mito (Sabaki, Galana) | Unyunyuziaji Maji<br>Kilimo | Mchanga mwingi unaosababisha mchanganyiko wa matope kutokanana na mmomonyoko wa udongo<br><br>Uharibifu mkubwa wa maeneo ya vyanzo vya maji<br><br>Wingi wa virutubisho kutokana na matumizi mengi ya mbolea zisizo za kawaida<br><br>Uondoaji usiodhibitiwa unaosababisha kupungua kwa mapato | Utalii wa kimazingira<br>- Nguvu za umeme<br>Vifaa vya kutibu taka<br><br>Matumizi ya mifumo ya kisasa ya unyunyiziaji maji.<br><br>Uboreshaji wa mitandao ya usambazaji maji. | Athari za hali za juu kwa mito<br><br>Kuongezeka kwa uchafuzi<br><br>Rasilimali chache za kifedha<br><br>Mafuriko ya mara kwa mara, uwekezaji wa gharama kubwa, | Uinzi wa mazingira ya miti<br>Kuanzisha taratibu za kupunguza mmomonyoko wa udongo k.m. ukarabati wa ukingo wa mto.<br><br>Fuatilia ubora wa maji mara kwa mara.<br><br>Kushughulikia usimamizi na uhifadhi wa vyanzo vya maji |
| Milima Mwangea | Maji<br>Utalii<br>Misitu<br>Kilimo | Uharibifu wa hali ya juu na uvamizi wa wanadamu | Chapisa kwenye Gazeti la serikali na kufanya ukarabati tendi | Ukame, uzalishaji wa mkaa na uvamizi wa binadamu | Utekelezaji wa sharia<br>Makundi ya usimamizi wa jamii |
| Maeneo yenye misitu (Dakacha) | Utalii<br>Kilimo<br>Misitu<br>Wanyama pori<br>Nishati | Uharibifu na uvamizi | Uchapishaji kwenye gazeti la serikali na kufanya ukarabati tendi | Uzalishaji wa makaa<br>Uvamizi wa wakulima majirani | Ushirikishaji wa jamii |
| Bahari | Uvuvi<br>Utalii<br>Wanyamapori<br>Elimu na utafiti | Uchafu wa baraini<br><br>Kuchafuliwa kwa mkondo wa maji<br><br>Kupungua kwa sekta ya uvuvi na utalii, | Kubali fursa za uwekezaji wa uchumi wa bahari | Uchafuzi wa maji,<br>Kupanda kwa viwango vya bahari | Uhamasishaji, ulinzi na usimamizi wa mfumo mzima wa ikolojia wa baharini, |

| Maliasili | Sekta tegemezi | Hali, kiwango cha matumizi, mtizamo wa siku zijazo | Fursa za matumizi bora | Vikwazo vya matumizi bora | Mikakati iliyopo ya usimamizi endelevu |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Uvamizi wa ufuo wa bahari | | Kufanya mwamba kutoka rangi | Mpango wa utekelezaji wa baharini wa Kenya, kanuni za BMU 2007 |
| Misitu (Kaya, Mikoko, ArabukoSokoke) | Kilimo<br>Uvuvi<br>Utalii<br>Afya<br>Ujenzi<br>Misitu | Uharibifu wa msitu, unaotumika kwa mambo ya kitamaduni,<br><br>Utumiaji wa kupita kiasi wa mfumo dhaifu wa ikolojia<br><br>Misitu Takatifu ya Kaya: Viwango vya juu vya ukataji miti na uharibifu | Imehifadhiwa kwa ajili ya utalii na urithi wa kitamaduni, kusudi takatifu<br><br>Uanzishwaji wa biashara asili, biashara ya kaboni, mahali penye rutuba ya kuzaliana samaki | Mitazamo hasi kuwa msitu wa kaya hutumika kwa matendo maovu<br><br>Ukame wa muda mrefu<br><br>Upungufu wa kisheria wa biashara ya kaboni, ukataji miti haramu, uvamizi na uchafuzi wa misitu ya mikoko unaofanywa na makampuni ya chumvi;<br><br>Upungufu wa fursa za ufadhili | Ukarabati wa msitu wa kaya uliofanywa na shirika la makumbusho ya kitaifa ya Kenya na serikali ya kaunti<br><br>Mpango wa kitaifa wa usimamizi wa mikoko, ushirikishwaji wa jamii kupitia biashara asili<br><br>Utekelezaji wa hali ya juu wa Sheria za Kitaifa za Mazingira (NEMA) pamoja na sheria zingine. |
| Rasilimali za madini (Manganizi, madini ya chuma, kokoto, matofali ya mwamba, madini ya Titanium, | Uzalishaji<br>Biashara<br>Ujenzi<br>Afya | Uchimbaji madini kusikothibitiwa<br><br>Maeneo ya uchimbaji madini ambayo hayajakarabatiwa | Uwepo wa malighafi nyingi za uzalishaji na ujenzi. | Takwimu duni juu ya hazina za madini na mahali zilipo.<br><br>Ukosefu wa sera ya uchimbaji wa rasilimali za | Idhini ya Kaunti ya uchimaji madini<br><br>Uhakiki wa ripoti za tathmini ya athari za mazingira |

| Maliasili | Sekta tegemezi | Hali, kiwango cha matumizi, mtizamo wa siku zijazo | Fursa za matumizi bora | Vikwazo vya matumizi bora | Mikakati iliyopo ya usimamizi endelevu |
|---|---|---|---|---|---|
| Chumvi, Mchanga) | | | | madini na manufaa ya jamii. | (EIA) kwa shughuli za uchimbaji madini,<br><br>Tengeneza kanuni za sanaa ya uchimbaji madini. |

## 2.8 Masuala ya Maendeleo

| Sekta | Swala la maendeleo | Sababu |
|---|---|---|
| Elimu | Upatikanaji mdogo wa mafunzo bora ya ufundi na elimu | Miundomsingi pungufu<br>Upungufu wa walimu wa mafunzo ya ufundi<br>Ukosefu wa ufahamu kuhusu programu za mafunzo ya ufundi (VT) kwa jamii<br>kazi inayohitaji ujuzi wa mikono na mafunzo maalumna programu zilizopitwa na wakati<br>Upungufu wa zana na vifaa vya kisasa vya mafunzo ya vyuo vya mafunzo ya ufundi(VTC) |
| | Upatikanaji mdogo wa elimu bora ya awali | Miundomisingi isiyofaa<br>Upungufu wa walimu wa elimu ya maendeleo ya watoto wachanga (ECDE) na wafanyakazi wenye ujuzi<br>Imani za kitamaduni na kidini za jamii<br>Ushuru wa elimu ya maendeleo ya watoto wachanga (ECD)<br>Ukosefu wa chakula katika manyumba<br>Vifaa duni vya kufundishia na kujifunzia<br>Ukosefu wa samani za kutosha<br>Ukosefu wa sera ya elimu ya awali katika kaunti<br>Rasilimali zisizotosheleza kujifunzia kidijitali |
| Maji, Mazingira na maliasili | Ukosefu wa upatikanaji wa maji safi na salama | Uharibifu wa mazingira<br>Miundomisingi duni ya maji<br>Usimamizi dhaifu wa maji<br>udunishaji duni ya miundomisingi ya maji<br>Kuegemea zaidi kwa umeme kwa usambazaji wa maji |
| | Huduma duni za kuondoa, maji machafu na takataka. | Miundombinu duni ya kuondoa, maji machafu na takataka.<br>Uelewa mdogo juu ya kuondoa, maji machafu na takataka. |
| | Uharibifu wa mazingira | Athari za Mabadiliko ya Tabianchi<br>Ukataji miti<br>Usimamizi dhaifu wa mazingira<br>Miundomisingi duni ya usimamizi wa taka<br>Uelewa duni wa Mazingira<br>Matumizi yasiyoendelevu ya maliasili<br>Kuongezeka kwa uchafuzi wa mazingira |
| Ardhi, Mipango tekelezi, Nyumba na Maendeleo ya Miji | Upungufu wa makazi bora na ya bei nafuu | Ukuaji wa makazi yasiyo rasmi na makazi duni<br>Miundombinu duni ya nyumba za bei nafuu<br>Uwekezaji mdogo katika miundombinu ya makazi<br>Utekelezaji duni wa udhibiti wa maendeleo |
| | Usimamizi na Utawala wa Ardhi | Usalama duni wa haki ya kumiliki mali<br>Upatikanaji duni wa habari na huduma za ardhi<br>Wavamiaji ardhi na wenye ardhi wasiokuweko |
| | Upungufu wa maendeleo na Mipango ya Miji | Uvamizi wa jamii kwenye hifadhi ya barabara na maeneo ya umma<br>Maendeleo yasiyodhibitiwa mijini na vijijini<br>Mipango duni ya maeneo ya makazi |
| Ukulima | Uzalishaji wa chini wa Mazao | Uegemeaji wa njia za jadi za kilimo<br>Kupungua kwa rutuba ya udongo<br>Upatikanaji duni wa pembejeo za kilimo zenye ubora wa bei nafuu<br>Ufikiaji duni wa huduma za nyanjani<br>Wadudu na magonjwa<br>Hasara kubwa baada ya mavuno<br>Miundo dhaifu ya uuzaji |
| | Uzalishaji wa chini wa mifugo | Upatikanaji duni wa vyakula bora vya mifugo kwa bei nafuu<br>Mbinu za ufugaji za kitamaduni |

| Sekta | Swala la maendeleo | Sababu |
| --- | --- | --- |
| | | Upatikanaji duni wa huduma za nyanjani za mifugo<br>Wadudu na magonjwa ya wanyama<br>Miundo dhaifu ya uuzaji wa bidhaa za mifugo |
| | Uzalishaji wa chini wa samaki | Miundomisingi duni ya uvuvi<br>Upatikanaji duni wa pembejeo za bei nafuu za ufugaji samaki<br>Upungufu wa uwezo wa wavuvi<br>Huduma duni za nyanjani<br>Upotevu mkubwa wa samaki baada ya kuvuliwa<br>Miundo dhaifu ya uuzaji wa samaki na mazao ya samaki<br>Usimamizi dhaifu wa rasilimali za uvuvi |
| Biashara, Utalii na Vyama vya ushirika | Ukuzaji na maenedelo ya biashara | Miundomisingi duni ya soko<br>Ukuzaji duni wa Biashara<br>Mazoea ya biashara yasiyo ya haki<br>Uwekezaji wa chini |
| | Ukuzaji na maendeleo ya utalii | Utangazaji duni wa utalii uuzaji wa Masoko<br>Ukosefu wa mafunzo na uhamasishaji<br>Miundomisingi duni katika maeneo ya vivutio vya watalii<br>Aina finyu ya bidhaa za Utalii |
| | Ukuzaji na maendelao ya vyama vya ushirika | Uelewa wa chini na demokrasia katika vyama vya ushirika<br>Usimamizi dhaifu katika Vyama vya Ushirika<br>Elimu, mafunzo na utafiti duni wa Vyama vya ushirika<br>Upungufu wamiundomisingi ya kutosha ya masoko ya Ushirika kwa ajili ya uongezaji thamani. |
| Nishati na miundomisingi | Upungufu wa mifumo ya Mtandao wa barabara na miundomisingi duni ya usafiri | Matengenezo na uimarihaji duni ya barabara<br>Miundomsingi duni ya mtandao ya barabara<br>Miundomisingi duni ya usafiri |
| | Ufikiaji wa chini wa nishati katika kaunti | Matengenezo na uimarishaji duni na maendeleo ya miundomisingi ya nishati<br>Uelewa duni juu ya nishati mbadala |
| Ulinzi wa jamii, Utamaduni na burudani | Upungufu wa huduma za ulinzi wa kijamii | Imani na desturi zilizopitwa na wakati<br>Huduma duni za ulinzi wa mtoto<br>Huduma/vifaa duni vya ulinzi wa kijamii<br>Kuongezeka kwa ukatili wa kijinsia (GBV) |
| | Uwezeshwaji mdogo wa Vijana / Ukosefu mkubwa wa ajira kwa vijana | Uwezo duni (ujuzi, mikopo nafuu) miongoni mwa vijana<br>Fursa chache za ajira<br>Utumiaji mbaya wa madawa ya kulevya / Huduma duni za urekebishaji |
| | Uhifadhi duni wa utamaduni na urithi | Kuzorota kwa utamaduni na urithi<br>Kutohifadhi maeneo ya kitamaduni<br>Uharibifu wa maeneo ya kitamaduni<br>Utetezi duni na uhamasishaji |
| | Maendeleo duni ya Michezo | Vifaa duni vya michezo<br>Uwezo duni wa maendeleo ya michezo |
| | Udhibiti dhaifu wa hatari na maafa | Miundomisingi duni ya kudhibiti maafa<br>Umahiri duni wa kibinadamu na kiufundi<br>Mfumo dhaifu wa usimamizi wa maafa<br>Utaratibu duni wa DRM usiotosheleza maonyo ya mapema<br>Uelewa mdogo wa hatari za maafa<br>Ustahimilivu dhaifu wa Jamii |
| Afya | Upatikanaji duni wa huduma za ukingaji na ukuzaji za afya | Huduma duni za za uzazi,Afya ya watoto wachanga, watoto na, na Vijana (RMNCAH)<br>Ufikiaji mdogo wa chanjo<br>Huduma duni za lishe |

| Sekta | Swala la maendeleo | Sababu |
|---|---|---|
| | | Huduma duni za uchunguzi (kifua kikuu, ukimwi, saratani, kisukari, shinikizo la damu, magonjwa ya akili na magonjwa mengine yanayoenezwa na wadudu)<br>Ufikiaji mdogo wa huduma za afya ya jamii |
| | Upatikanaji wa huduma duni za Tiba na Urekebishaji | Ukosefu wa huduma za matibabu<br>Huduma duni za urekebishaji.<br>Upungufu wa huduma maalum za afya kwa mfano, madaktari wa saratani, usafishaji damu kwa mashine ya figo. n.k<br>Mfumo dhaifu wa rufaa |
| | Usimamizi wa Afya na Huduma saidizi | Uwezo duni wa Rasilimali ya Watu<br>Upungufu wa miundomisingi na vifaa vya afya<br>Pengo katika usimamizi na uratibu<br>Bidhaa na teknolojia duni za kiafya<br>Ufikiaji mdogo wa afya kwa wote |
| Utawala wa Umma na Mahusiano ya Serikali | Usimamizi wa fedha za umma | Kiwango cha chini cha matumizi<br>Mapato ya chini ya vyanzo vya kaunti<br>Mifumo dhaifu ya udhibiti wa ndani<br>Uwezo duni wa kuandaa Bajeti |
| | Upangaji dhaifu wa Sera, uratibu na ufuatiliaji na utathmini | Utendaji dhaifu wa ufuatiliaji na utathmini<br>Upungufu wa huduma za mipango ya Uchumi na uratibu<br>Uwezo duni wa takwimu za kaunti |
